




- Unyevunyevu unatarajiwa kuongezeka kutokana na mvua za *Masika* na *Msimu* zinazoendelea
- Unyevunyevu uliokithiri unaweza kuathiri mazao hasa yaliyopo mabondeni
- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani na kutumia taarifa za hali ya hewa katika shughuli zao za kila siku

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2020

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliimarika. Hali hii ilisababisha ukanda wa mvua kusukumwa kuelekea kaskazini mwa nchi. Uwepo wa Joto la bahari la juu ya wastani katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Madagascar) lilisababisha kutokea kwa migandamizo midogo ya hewa. Katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kulikuwa na joto la bahari la juu ya wastani, hali iliyopelekea kuwa na mchango mdogo katika kuleta upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuja kwenye baadhi ya maeneo ya nchi yetu. Hata hivyo uwepo wa ukanda wa mvua ulichangia kuongezeka kwa mvua hususani katika baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua.

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2020

Mifumo ya hali ya hewa ilichangia uwepo wa mvua katika maeneo mengi ya nchi ambapo kiasi cha mvua cha kati ya mm 26 hadi mm 200 kilirekodiwa. Katika maeneo kusini mashariki mwa mkoa wa Morogoro na magharibi mwa Ruvuma, yamepata kiasi cha mvua zaidi ya mm 200 kama inavyoonekana katika kielelezo.



Kielelezo : Kiasi cha mvua katika kipindi cha Machi 21-31, 2020

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2020

Katika dikadi hii, maeneo mengi ya nchi yamepata ongezeko la mvua ingawa baadhi ya maeneo ya Dodoma, Singida, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Morogoro, Rukwa na Mbeya yamepata unyevunyevu uliokithiri ambao unaweza kusababisha athari katika shughuli za kilimo. Zao la mahindi katika maeneo mengi yanayopata msimu wa mvua mara moja kwa mwaka lipo katika hatua ya kukomaa. Wakulima katika mikoa

ya Iringa, Njombe, Singida na Ruvuma walikuwa wanaendelea na uvunaji wa maharagwe, kwa mkoa wa Mbeya waliendelea na upandaji wa maharagwe. Kwa maeneo machache ya mkoa wa Iringa na Njombe wakulima walikuwa wanaendelea na uvunaji wa viazi mviringo. Kwa upande wa maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka, wakulima waliendelea na shughuli za kupanda mahindi na maharagwe. Aidha, mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Simiyu wakulima waliendelea na uvunaji wa mahindi ya msimu wa vuli yaliyopandwa kwa kuchelewa. Maeneo machache ya ukanda wa pwani ya kaskazini (Morogoro, Tanga, na visiwa vya Pemba, na Unguja) zao la mpunga lilikuwa katika hatua ya kutoa maua.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2020

Kiwango cha maji katika mabwawa na kutiririka kwa maji katika mito vimeongezeka katika maeneo mengi ya nchi kutokana na mvua za *Masika* na *Vuli* zinazoendelea.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2020.

Katika kipindi hiki, mifumo ya migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu kidogo wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kuongezeka nguvu kidogo. Hali hii itapelekea ukanda wa mvua kusukumwa kidogo kuelekea kaskazini mwa nchi. Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea kuwepo katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi pamoja na kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) na kusababisha vipindi vya migandamizo midogo ya hewa kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Kwa upande mwingine, upepo hafifu unatarajiwa kuvuma kutoka magharibi kuelekea maeneo ya nchi yetu, hivyo kuwa na mchango mdogo katika kuimarisha mifumo ya kutengeneza mvua kutoka katika misitu ya Congo. Hali hii inatarajiwa kuendelea kuimarisha ukanda wa mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani, nyanda za juu kusini magharibi pamoja na baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki.

HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2020.

Maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) yanatarajiwa kupata mvua za wastani katika baadhi ya maeneo hususan nusu ya kwanza ya dekadini.

Kanda ya ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kupata mvua za wastani katika baadhi ya maeneo hususan nusu ya pili ya dekadini.

Kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na kusini mwa Morogoro) na pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajiwa kupata mvua za wastani katika baadhi ya maeneo .

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) na magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kupata mvua katika maeneo machache.

Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) na Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) yanatarajiwa kupata mvua nyepesi katika maeneo machache.

HALI YA HEWA KILIMO INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2020

Mvua za Masika na Msimu zinazoendelea kunyesha zitasaidia kuongeza unyenyevu kwa ajili ya ukuaji wa mazao. Hata hivyo mazao yaliyopo mabondeni yanaweza kuathirika kutokana na unyenyevu uliokithiri na mafuriko hususan katika maeneo ya mikoa ya Dodoma, Singida, Dar es salaam, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Morogoro, Rukwa na Mbeya. Wakulima wanashauriwa kuchukua hatua na kutumia njia bora za kilimo ili kuepusha mazao yasiathirike na unyenyevu uliokithiri katika maeneo ya mabondeni. Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani na kufuatilia taarifa za hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini kwa ajili ya shughuli zao za kila siku.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2020

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo, watumiaji wa maji wanashauriwa kuendelea kuyatumia kwa uangalifu na kuchukua tahadhari juu ya majanga yaletwayo na mafuriko.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

Ghorofa ya 3-Ubungo Plaza – 388 Barabara ya Morogoro,

S.L.P 3056; 16102 Dar es Salaam, Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti:

www.meteo.go.tz, -Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania